

**Harakati za Kuipinga Jumuiya ya Ahmadiyya ndani ya Uislamu**

**13 Septemba 1999**

Al Hamdulillah Wahdahu wa AsSalaatu wa AsSalaamu 'ala mun La Nabiya Ba'adahu

*Sifa zote njema ni za Mwenyezi Mungu, Aliyepwekeka, na Mapenzi na Rehema  
Zake zimshukie Yule ambaye baada yake hakuna tena Nabii.*

**'Acheni mawasiliano yote na Dkt. Rashid na Mulla Irshad.' Hivi ndivyo Mirza  
Tahir anavyowaamrisha wafuasi wake**

Alhamdulillah, Ukweli unapodhihiri, uongo hutoweka!

Ilikuwa ni mwanzoni mwa mwaka 1996 pale jamaa mmoja kutoka Sweeden aliponizindua kuwa kulikuwa na ushawishi wa kufanya watu waukubali ukadiani uliokuwa ukiongezeka kwa kiasi kikubwa katika mtandao wa intaneti. Wakati huo mimi nilikuwa hata sijui hiyo intaneti ndiyo nini. Hakukuwa na kitu cha aina hiyo katika Falme za Kiarabu.

Lakini muda mfupi baada ya huduma hii ya intaneti kuingia huku ndipo nilipogundua kuwa kweli Makadiani walikuwa wakitumia sana tovuti, walikuwa na tovuti kadhaa tofauti, mara nyingi, wakitumia jina la Uislamu, lakini chache zilitumia jina la Ahmadiyya.

Walikuwa wakitumia sana fursa za mijadala ambapo kama kawaida yao walijidai wao ndio watetezi wa Uislamu. Baadhi ya tovuti zao zilikuwa zikifanya kazi chini ya mwamvuli wa Uislamu na nyingine chini ya anuani ya Ahmadiyya. Wakatamba sana kiasi kwamba walithubutu hata kutuma mtandaoni tafsiri za baadhi ya maandiko ya Mirza Ghulam A. Qadiani.

Tahamaki, kwa Rehema za Mwenyezi Mungu, na sisi tukaanzisha ukurasa wa Harakati za Kupinga Jumuiya ya Ahmadiyya ndani ya Uislamu katika tovuti ili kukabiliana na propaganda za Makadiani na kuwapa watu mwamko wa kufahamu itikadi ya Jumuiya ya Ahmadiyya kwa jina la Uislamu.

Makala kadhaa zikawekwa kwenye tovuti hiyo zikianika hadharani tabia za Mirza Ghulam, maisha yake na imani zake zinazopingana na Uislamu, zikinukuu kwa kiasi kikubwa vitabu vya Mirza Ghulam Ahmad Qadiani na vyanzo vingine vya Ukadiani. Tangu mwanzo kabisa tulianzisha mawasiliano na tovuti mbalimbali za Makadiani ili umma usikie pande zote mbili.

Ukurasa wa guestbook ni kielelezo cha mafanikio ya tovuti hii na athari uliyonazo kwa Jumuiya ya Ahmadiyya. Baruapepe zenye matusi kutoka kwa Makadiani ndizo zilizotawala kila siku.

Majaribio kadhaa yalifanywa ili kuihujumu tovuti hii na kuiharibu kompyuta yangu kwa virusi na zana nyingine za siri katika vyumba vya guestbook. Lakini mwanadamu anapanga, Mungu anapangua. Maudhui katika tovuti yangu ni

dhahiri yaliwatatiza wafuasi wa Qadiani/Ahmadiyya na uongozi wao. Tulikuwa tunatumia baadhi ya maudhui katika tovuti ya Makadiani, kuthibitisha jinsi maelezo ya msemapeka yalivyokuwa yaktumika kuudanganya umma.

Hatimaye mwaka jana, Tovuti zote za Makadiani zikafungwa kwa maagizo ya Mirza Tahir, Amiri wa Jumuiya ya Ahmadiyya, kwa kisingizio cha kuziboresha. Mawasiliano ya Makadiani katika tovuti yangu ndiyo yamebaki ukumbusho wa tovuti hizo.

Tovuti pekee rasmi ya Makadiani inayofanya kazi ina hotuba mbili za Mirza Tahir. Nilipouliza sababu ya mabadiliko haya, mmoja wa wanaharakati wa Qadiani katika intaneti, Farhan Qureshi na baadhi ya Makadiani wengine waliniambia kuwa eti sisi tulikuwa tukitumia maandiko kutoka kwenye tovuti hizo za Qadiani, tukiyapinduapindua au kuyapotosha ili kutengeneza maudhui ya kuwapinga Ahmadiyya.

Mimi nikawashauri kwamba kwa hali hiyo basi kuna haja ya kuyaacha maandiko hayo kwenye tovuti ili watu wabaini jinsi mimi nilivyo mwongo mkubwa, jinsi nisivyokuwa mwadilifu!! Kisha nikawaauliza sababu ya kubakisha hotuba tu za Mirza Tahir katika tovuti. Jibu lao likawa: eti ni vigumu kwetu kuelewa maana ya maandiko ya Mirza Ghulam na hotuba za Mirza Tahir kwa njia nyepesi-nyepesi ya kuyaelewa!!

Kufuatia kuzipiga mweleka tovuti za makadiani, wanaharakati hawa wa Kadiani wakashughulika zaidi na fursa mbalimbali za mijadala. Hata hivyo, hivi sasa mwelekeo wao umebadilika kutoka ule wa ushawishi wa hoja za nguvu za kuwaingiza watu katika ukadiani kuja katika utetezi wa hovyo wa kumuhami kiongozi wao mwasisi na itikadi zake za uzushi.

Lakini hakukuwa na kikubwa ambacho wangeweza kufanya kuhusiana na maandiko ya Mirza Ghulam. Hawawezi kukanusha kuwepo kwa vitabu hivyo na hawawezi kukanusha nukuu kutoka vitabu hivyo. Utetezi bora zaidi ambao wangeufanya ulikuwa uwe kama ifuatavyo:

Kuepuka na kuacha jitihada za kujadili wasifu wa Mirza Ghulam na maandiko yake

Kubainisha mapenzi ya Mirza kwa Allah, Mtume Mtukufu, Qur'an na Hadith

Kujaribu kuendeleza majadiliano juu ya masuala ya kitikadi kuhusu Mwisho wa unabii, maisha/kifo/kupaa kwa Yesu n.k. Kwa maneno mengine waendeleze majadiliano juu ya Qur'an na Hadith na kuacha kumjadili Mirza na Vitabu vyake.

Wakanushe usahihi wa nukuu

Waendelee kutoa hoja kuwa nukuu zimetoka nje ya muktadha, kwamba maana zimegeuzwa n.k.

Maana halisi ni za kitamathali kwa undani wake

Wabadili mada

Wanyamaze kimya na kutumai kuwa hatari itapita

Vyovyyote iwayyo, jitihada zangu na jitihada za kudumu za jamaa mwingine wa Marekani (Irshad) za kufichua udanganyifu wa Mirza Ghulam, na mapambano yasiyokoma dhidi ya wanaharakati wa Qadiani katika mitandao ya intaneti hatimaye zimemlazimu Mirza Tahir kutoa amri nyininge: Acheni mawasiliano na Dkt. Rashid na Mullah Irshad kwenye Intaneti.

Kuna sababu ya hatua hiyo. Viongozi kama Mirza Tahir wao hudumisha njia ya mawasiliano ya upande mmoja na wafuasi wao. Yeye hataki wafuasi wake kushiriki katika njia ya majadiliano ya pande mbili na wapinzani wa Ahmadiyya. Njia zote zile ambazo kwazo aina hii ya mawasiliano huwezekana huepukwa huku wafuasi, wakati mwingine, wakikatazwa kushiriki, au kulazimishwa kuepuka aina hii ya midahalo/mijadala.

Mtandao wa intaneti umetoa fursa ya aina yake kwa watu kuwasiliana, iwe mara nyinyi au mara chache katika muda muafaka. Ahmadiya/Makadiani wengi wamekuwa wakigundua mambo mengi kuhusiana na maoni ya wapinzani wa Ahmadiyya ambapo kwa mara ya kwanza katika maisha yao wamesoma maandiko ya Mirza Ghulam ambayo hapo kabla hawakuwa na uwezekano wa kuyapata.

Bila shaka, matokeo ya mawasiliano hayo ni kwamba sehemu kubwa ya vizazi vipyta vyta Ahmadiyya vimeanza kuuliza maswali mengi kuhusu ukweli halisi. Na jambo hili limekosa uvumilivu wa uongozi wa Kadiani, kwa sababu wanajua athari zake. Linaweza kuifutilia mbali hadithi yote ya Ahmadiyya

Ndiyo sababu ya Mirza Tahir kusema: Acheni mawasiliano yote na Dkt. Rashid na Mulla Irshad katika mtandao wa intaneti.

Masikini wee Mirza Tahir!! Mbona kachelewa. Wimbi linageuka na IshaAllah muda si mrefu uongo wote huu utafika kwenye hitimisho lake la kimantiki-Jaa alHaq wa zahaq albaatil-Ukweli unapokuja, uongo hutoweka.

. Wassalam 'ala mun ittaba'a alhuda

Dr. Syed Rashid Ali

rasyed@emirates.net.ae

<http://alhafeez.org/rashid/>